

Gumzo la RCS

Jibe Mobile Ltd. ("Jibe Mobile")

70 Sir John Rogerson's Quay, Dublin 2, Ireland

<https://support.google.com/>

Ilisasishwa tarehe 16 Machi, 2023

Toleo la awali: [Tarehe 21 Desemba, 2020](#)

Muhtasari wa mkataba

- Muhtasari huu wa mkataba unaelezea vipengele vikuu vya ofa ya huduma yetu kama inavyotakiwa na sheria ya Umoja wa Ulaya¹.
- Imekusudiwa kukusaidia kulinganisha kati ya ofa za huduma.
- Maelezo kamili kuhusu ofa yetu ya huduma yanapatikana kwenye hati nyingine.

Huduma

Gumzo la RCS hutoa hali ya utumiaji iliyosasishwa na inayofaa ya utumaji wa ujumbe kwa watumiaji wa Programu ya Messages kutoka Google. Muunganisho wa intaneti unahitajika ili kutuma ujumbe wa Gumzo la RCS. Gumzo la RCS hutolewa na Jibe Mobile kwa kutumia ustadi na umakini unaofaa, ingawa hakuna viwango vya chini vya ubora wa huduma vinavyotolewa.

Bei

Gumzo la RCS hutolewa bila malipo na matumizi yake ni kwa mujibu wa Masharti ya Huduma ya Simu ya Jibe (yanayopatikana katika <https://jibe.google.com/policies/terms/>) na Sheria na Masharti ya Google (yanayopatikana katika <https://policies.google.com/terms>).

Muda, usasishaji na kusimamisha

Gumzo la RCS linapatikana ili ulitumie papo hapo baada ya kujisajili. Hujajitolea kutumia Gumzo la RCS kwa muda usiobadilika na uko huru kuacha kulitumia wakati wowote.

Vipengele vya watumiaji wa hatima walio na ulemavu

Unaweza kutumia kisoma skrini kwenye Gumzo la RCS. Maelezo zaidi yanapatikana katika <https://support.google.com/messages/answer/6105764?hl=en>.

Maelezo mengine yanayofaa

Usaidizi kwa Wateja: Usaidizi wa Gumzo la RCS unapatikana kwenye <https://support.google.com/>.

Mabishano: Unaweza kupeleka malalamiko kwa mto huduma wa mbinu mbadala ya utatuzi wa mzozo aliyeorodheshwa kwenye <https://ec.europa.eu/consumers/odr/main/?event=main.adr.show2> au mto huduma mwengine, kama inavyotakiwa kisheria kwenye nchi uliko. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye Sheria na Masharti ya Google.

Matukio ya Kiusalama: Jibe Mobile hudumisha mpango madhubuti wa usimamizi wa matukio wakati wowote ili kutambua na kujibu matukio ya usalama au ya faragha bila kuchelewa. Pia, Jibe Mobile hutoa Orodha Hakikishi ya Usalama ili kukusaidia kudhibiti usalama wako wa mtandaoni.

¹ Makala ya 102(3) ya Agizo (EU) 2018/1972 la Bunge la Ulaya na Baraza la tarehe 11 Desemba, 2018 lililoweka Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki ya Ulaya (OJ L 321, 17.12.2018, uk. 36).

Data Binafsi: Ili kujisajili kwenye Gumzo la RCS, unahitaji kutoa nambari yako ya simu. Sera ya Faragha ya Google (inapatikana katika <https://policies.google.com/privacy>) inatoa maelezo zaidi kuhusu data binafsi inayokusanywa na Jibe Mobile unapotumia Gumzo la RCS. Sera ya Faragha ya Google si sehemu ya mkataba kati yako na Jibe Mobile au ya muhtasari huu.